LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# MABARAZA YA USULUHISHI WA NDOA

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

# MABARAZA YA USULUHISHI WA NDOA

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO

SHUKRANI ........................................ 5
DIBAJI ........................................ 5
UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU ........................................ 7
MAONO ........................................ 8
TAMKO LA LENGO MAHUSUSI ........................................ 8
LENGO KUU ........................................ 8
1. Utangulizi. ........................................ 9
2. Mabaraza ya usuluhishi wa ndoa. ........................................ 10
3. Idadi ya wajumbe katika baraza. ........................................ 11
4. Mamlaka ya baraza katika kupokea migogoro ya ndoa. ........................................ 11
5. Taratibu za kufuatwa katika usuluhishi wa migogoro ya ndoa. ........................................ 12
6. Mazingira yanayoweza kupelekea mgogoro wa ndoa kutopitia baraza la usuluhishi. ........................................ 15
7. HITIMISHO ........................................ 17

## SHUKRANI

Tunatoa shukrani za dhati kwa mwanasheria wetu Wakili Hamisi Mayombo pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu hususani ofisi ya Arusha kwa kukiandaa kijitabu hiki.

## DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote

kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndiyo maana basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi wa kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia.

Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako kupata usaidizi huu.
**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.**

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo yapo Dar es Salaam. Pia Kituo kina ofisi nyingine Arusha na Dodoma.Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria

# 1. Utangulizi.

Kumekuwa na changamoto kubwa katika utatuzi wa migogoro ya ndoa katika nchi yetu. Hii inatokana na ukweli kwamba watu wengi hawafahamu sheria na taratibu za kufuata endapo mgogoro unapotokea. Sheria ya ndoa ya mwaka 1971 imeweka wazi taratibu za kufuata pale wanandoa wanapoingia kwenye mgogoro na kuamua kutaka kuvunja ndoa hiyo. Sheria inataka migogoro hiyo kufikishwa mbele ya mabaraza ya usuluhishi kwanza kabla ya kupelekwa mahakamani. Mgogoro wa ndoa hupelekwa mbele ya mahakama tu pale inapotokea baraza la usuluhishi limeshindwa kusuluhisha. Kijarida hiki kimedhamiria kueleza kwa lugha nyepesi maana ya mabaraza ya ndoa, nguvu yaliyo nayo kisheria, kazi zake, taratibu za usuluhishi na mazingira yanayoweza kupelekea muomba talaka kupeleka mgogoro moja kwa moja mahakamani bila kupitia kwenye baraza la usuluhishi.

## 2. Mabaraza ya usuluhishi wa ndoa.

Kwa mujibu wa kifungu cha 102 cha Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 Waziri wa Katiba na sheria amepewa mamlaka ya kuanzisha mabaraza ya usuluhishi wa ndoa kwenye kila kata katika nchi au eneo lolote kadri ya uhitaji wa eneo husika. Kama jamii fulani imeanzisha kamati inayojihusisha na utatuzi wa migogoro ya ndoa na waziri akajiridhisha kuwa kamati hiyo inaweza kufanya hivyo, basi waziri ataitangaza kamati hiyo kuwa ni baraza la usuluhishi wa ndoa katika jamii hiyo linalotambulika kisheria. Kwa sasa Tanzania mabaraza ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa yanayotambulika ni mabaraza ya kata, Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA). Baraza la kata limekuwa likisuluhisha migogoro yote ya ndoa zilizofungwa kimila, kiserikali na kidini hususani ndoa za Kikristo; na BAKWATA imekuwa ikijishughulisha na usuluhishi katika migogoro ya ndoa zilizofungwa kwa mujibu wa taratibu za Kiislamu. Lakini vilevile lazima itambulike

kwamba migogoro ya ndoa iliyofungwa kikristo au dini nyingine inaweza kupelekwa kwenye makanisa husika kwa usuluhishi.

## 3. Idadi ya wajumbe katika baraza.

Kila baraza la usuluhishi wa migogoro ya ndoa linatakiwa kuwa na Mwenyekiti pamoja na wajumbe wasiopungua wawili na wasiozidi watano. Inashauriwa mwanamke awepo japo mmoja kati ya wajumbe kwenye baraza hilo japokuwa sheria iko kimya. Hii ina maana kwamba ukiacha Mwenyekiti, baraza linatakiwa kuwa na wajumbe wengine wasiopungua wawili na wasiozidi watano.

## 4. Mamlaka ya baraza katika kupokea migogoro ya ndoa.

Mgogoro wa ndoa utatakiwa kupelekwa au kufunguliwa kwenye baraza lililopo kwenye kata ambayo mume au mke anaishi au kama

itatokea mume au mke siyo mkazi wa Tanzania basi mgogoro huo utafunguliwa kwenye baraza lililoko kwenye kata ambayo mume au mke anaishi. Vilevile, kama wanandoa wanatoka kwenye jamii moja na jamii hiyo ina kamati inayotambulika na waziri katika utatuzi wa migogoro ya ndoa basi mgogoro unaweza kupelekwa katika baraza la jamii hiyo.

## 5. Taratibu za kufuatwa katika usuluhishi wa migogoro ya ndoa.

Baraza ambalo mgogoro wa ndoa umepelekwa litahitajika kuwaita wahusika wote wa mgogoro yaani wanandoa kufika barazani. Baraza pia litatakiwa kuhakikisha pande zote mbili yaani mume na mke, kila mmoja anapatiwa nafasi ya kusikilizwa. Sheria pia inalipa baraza uwezo wa kumuita mtu mwingine yeyote katika usuluhishaji huo pale litakapoona inafaa. Mtu huyo anaweza kuitwa barazani endapo baraza litahitaji kujiridhisha na baadhi ya mambo

yanayohusiana na mgogoro husika.
Kama baraza litamhitaji mtu kufika barazani basi litatakiwa kumpelekea wito wa maandishi utakaoonesha muda, sehemu na siku ya kufika barazani. Kama itatokea mtu amepuuza wito huo basi baraza litafanya maombi katika mahakama ya wilaya au ya mwanzo ili kutoa wito (samansi) kwa mtu huyo kufika barazani katika muda, siku na sehemu itakayotajwa katika wito huo (samansi). Ikumbukwe wito (samansi) huo ambao mhusika ataitiwa kupitia mahakama utatambulika kama wito halali wa mahakama kama pale inapomuita shahidi kwenye shauri. Kama mhusika atapuuza wito huo basi atakuwa amedharau wito halali wa mahakama kitendo ambacho ni kosa kisheria na ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria.

Kama itatokea baraza limeshindwa kusuluhisha mgogoro wa ndoa kwenye kiwango ambacho wahusika wenyewe wangeridhia, baraza litahitajika kutoa cheti kitakachoonesha mgogoro huo umeshindikana kusuluhishwa.

Pamoja na cheti hicho cha usuluhishi baraza kwa hiari yake linaweza kuambatanisha mapendekezo ambayo lenyewe litaona yanafaa au yanahusiana na mgogoro huo.

Sheria inakataza mawakili kuwawakilisha wahusika wa mgogoro katika baraza la usuluhishi wa migogoro ya ndoa. Vilevile sheria inakataza mwakilishi wa aina yoyote katika usuluhishi isipokuwa mwanafamilia na ni pale tu atakaporuhusiwa na baraza.

Ukiachilia mbali taratibu zilizowekwa na sheria ya ndoa ya mwaka 1971 na kanuni zingine zilizotungwa kutokana na sheria hii, kila baraza litakuwa likijiwekea taratibu zake za kuendesha usuhulishwaji wa migogoro ya ndoa.

## 6. Mazingira yanayoweza kupelekea mgogoro wa ndoa kutopitia baraza la usuluhishi.

Kama ilivyooneshwa hapo juu kwamba hakuna maombi ya talaka yatakayopelekwa mahakamani bila ya kupitia kwenye baraza la usuluhishi. Lakini Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inaweka mazingira yatakayopelekea mgogoro wa talaka kwenda mahakamani moja kwa moja bila kupitia kwenye baraza la usuluhishi.

**Mazingira hayo ni kama yafuatayo;**

1. Pale muomba talaka atakapothibitisha mbele ya mahakama kwamba mume au mke wake amemtelekeza kwa muda mrefu na hajui na wala hana taarifa zozote ambazo zinaeleza sehemu ambayo mwenza wake yupo.
2. Pale ambapo mume au mke ambaye maombi ya talaka yameombwa dhidi yake anaishi nje ya nchi na hakuna matarajio yoyote ya kurudi nchini ndani ya miezi

sita toka siku ambayo maombi ya talaka yameombwa.

3. Pale ambapo mume au mke ambaye talaka imeombwa dhidi yake, ameitwa mbele ya baraza la usuluhishi na kwa makusudi akakataa kufika mbele ya baraza.
4. Pale ambapo mke au mume ambaye talaka imeombwa dhidi yake amefungwa jela kwa kipindi cha miaka mitano au zaidi. Au amewekwa kizuizini na sheria ya vizuizi kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita.
5. Paleambapomuombatalakaanapotuhumu kwamba mke au mume ambaye talaka imeombwa dhidi yake anaumwa ugonjwa wa akili ambao hautibiki.
6. Pale ambapo mahakama imejiridhisha kwamba mazingira ya mgogoro yana upekee na utofauti mkubwa hivyo hata ukipelekwa kwenye baraza la usuluhishi wa ndoa haitakuwa na tija wala kusuluhika.

# 7. HITIMISHO

Hivyo basi, ni lazima ifahamike kwamba mabaraza ya usuluhishi wa ndoa yapo kisheria na kazi yake kubwa ni usuluhishi tu na siyo vinginevyo. Hivyo kama baraza limeshindwa kuwasuluhisha wanandoa basi litatoa cheti cha kuonesha kuwa usuluhishi umeshindikana. Baada ya hapo mke au mume hatahitajika kukata rufaa bali kufungua shauri jipya mahakamani huku akiambatanisha cheti hicho cha usuluhishi. Vilevile lazima ikumbukwe kwamba baraza la usuluhishi wa migogoro ya ndoa siyo chombo cha maamuzi, kwani hayana uwezo wa kutoa talaka wala amri zingine zozote zaidi ya kusuluhisha tu.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU (MAKAO MAKUU)**
Jengo la Jaji Lugakingira,
S. L. P. 75254, Kijitonyama, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz
**Tovuti:** www.humanrights.or.tz

**KITUO CHA MSAADA WA SHERIA**
Mtaa wa Isere - Kinondoni, S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

**OFISI YA ARUSHA**
Barabara ya Olerian, Olosiva, Kitalu Na. 116/5, Sakina kwa Idd,
S. L. P. 15243, Arusha – Tanzania **Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**OFISI YA DODOMA**
Kitalu na 22. Area D, S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV